

Jinsi ya kutumia huduma za ukalimani



scottish
refugee
council

Aprili 2011

How to use interpreting services - Swahili



Wakalimani ni wataalamu waliohitimu katika lugha ambazo pia wanaweza kuhakikisha kuwa mawasiliano kati yako na wafanyakazi wetu wa kesi yanaeleweka iwezekanavyo.

Hii ni muhimu hasa unapotoa tondoti kuhusu sababu yako ya kutafuta kimbilio. Ukalimani hukusaidia kupunguza kuchanganyikiwa au kutoelewana. Hatupendekezi hata kidogo utumizi wa marafiki au marafiki au familia kwa ukalimani kwa sababu hawajajifunza jinsi ya kuwasiliana na lugha . kwa hivyo, wanaweza kutokuwa na ujuzi wa kujieleza dhahiri unachosema, nah ii inaweza kusababisha kutoelewana.

Tutapanga mkalimani kwa ajili yako iwapo tunafikiri kuwa mawasiliano kati yako na wafanyakazi wetu hayaeleweki au hayafanyi kazi vyema. Iwapo ungependa lugha fulani tafadhali tueleze na tutajaribu kutatua tatizo hili.

Hupaswi kuulizwa kugharamia mkalimani na unapaswa kuripoti jambo hili mara linapotukia.

Haki na Majukumu

Mkalimani aliyetolewa lazima aelewe na kuongea lugha unayotaka. Kupata mkalimani anayeongea lugha yako inaweza kuwa jambo gumu la kupanga; hata hivyo una haki ya kupata mkalimani ambaye ni :

- Muadilifu – hatajaribu kuathiri unachosema au kutokuelewa
- Mstadi – mara nyingi anayetafsiri jna kwa jina na habadilishi maana ya jambo unalowaeleza
- Mtaalamu – anakuheshimu kama binadamu, pamoja na usiri na hakiuki ufaragha au kutoa maelezo uliyowaeleza kwa watu wa nje
- Habagui – hufanya mambo kwa njia isiyokubagua dhidi ya uraia wako, asili, imani (kidini au za kisiasa), jinsia, muelekeo wa kingono, masuala ya umri au afya

Iwapo ungependa, unaweza kuuliza kupata mkalimani wa kiume au wa kike. Tutaifanya tuwezavyo ili kufadhili ombi lako; tunaweza kutafuta mkalimani binafsi au kwa njia ya simu.

Migongano ya mapendeleo

Iwapo mkalimani wako ametafsiri kwa shirika lingine au anakujua kutoka kwa jumuiya yako na amekuwa kama mshauri wako au rafiki, basi hili linapaswa kutambulishwa kwa mfanyakazi wa kesi yako na mkalimani na pia wewe,

Iwapo huwezi kuhudhuria miadi yako

Sisi ni wafadhili walio na fedha chache. Iwapo utachelewa au kukosa kwenda kwa miadi yako na tumepanga mkalimani, bado itatubidi kulipa.

Iwapo utaendelea kukosa kuhudhuria miadi na huyafutilii, hatutaweza kutoa huduma za ukalimani kwako.

Iwapo huwezi kuhudhuria miadi yako, tupigie simu katika **0800 085 6087** ili kuyafuta (simu ni za bure kutoka kwa simu za nyaya, sio simu za mkono).

Jinsi ya kutoa malalamiko au pendekezo

Mkalimani hutoa usaidizi wa mawasiliano. Wakalimani sio washauri; ni kinyume cha sheria kwao kutoa ushauri wa uhamiaji au wa utafuta kimbilio.

Iwapo hufurahii huduma ambayo mkalimani wako anatoa, au ungependa kutoa pendekezo lolote, lazima ujulishe mfanyakazi wa kesi yako au mfanyakazi mmoja wa Halmashauri ya wakimbizi ya Uskoti mara moja.

Iwapo lalamiko lako haliwezi kutatuliwa, unaweza kufanya lalamiko lililoandikwa kwa kukamilisha fomu ya malalamiko inayopatikana katika ofisi au tovuti yetu:

http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/assets/0000/0183/Complaint_leaflet_English_March_2010.pdf

au uwasiliane nasi kupitia njia ya tovuti yetu katika:

<http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/contact>

Fomu yako ya malalamiko iliyokamilika inapaswa kurejeshwa kwa ofisi yetu.

Mapendekezo yako pia yanakaribishwa na yanaweza kuwasilishwa kwa kisanduku chetu cha mapendekezokilicho katika ofisi yetu.

Iwapo unahisi umepokea ushauri mbaya au huduma isiyofaa, unaweza kulalamika kwenye Ofisi ya Kamishna wa Uhamiaji (OISC): <http://www.oisc.gov.uk/>